


Mkulima Mbunifu

Jarida la kilimo endelevu Afrika Mashariki



Toleo la 64, Januari 2018

Mipango thabiti hutimiza malengo



Picha: MKM

Katika maisha, kila jambo au lengo linalotarajiwa kufanyika huhitaji mipango thabiti ili liweze kutimia, na endapo unategemea kulifanya bila kuwa na mpangilio uliokamilika, basi ni hakika jambo hilo kamwe haliwezi kutimia.

Ikiwa tunaanza mwaka mpya wa 2018, tunaamini kuwa kama mkulima na mfugaji, kuna malengo mengi umeweka kwa ajili ya safari hii mpya. Hakikisha kuwa, yale uliyoshindwa kuyatimiza kwa mwaka uliopita, basi

unaweka juhudi katika malengo hayo mwaka huu, na zaidi angalianjia ambazo utazitumia ili uweze kuyatimiza kwani changamoto ulizopata ni moja ya njia ya kukufanikisha,

Mkulima Mbunifu, tutaendelea kukupa elimu stahiki na inayozingatia misingi ya kilimo hai kwa mwaka huu wote, lakini pia tunakutakia mwaka mpya wenye mafanikio tele katika uzalishaji na hata usindikaji wa mazao yako.

Zaidi soma Uk 4 & 5 ➔

Fahamu kuhusu ugonjwa wa ndui ya mbuzi

Ufugaji wa mbuzi wa kienyeji na wa kisasa hasa kibiashara umekuwa kwa kiasi kikubwa tofauti na miaka ya nyuma lakini suala la magonjwa limekuwa likiathiri sana uzalishaji huu hata kupelekea wafugaji wengine

MkM kwenye mtandao

Njia ya mtandao yaani internet, inawasaidia wale wote ambao hawana namna ya kupata machapisho ya Mkulima Mbunifu moja kwa moja, kusoma kwenye mtandao na hata kupakua nakala zao wao wenyewe.



[mkulimambunifu.org](http://www.mkulimambunifu.org)
<http://issuu.com/mkulimambunifu>




<http://www.facebook.com/mkulimambunifu>



<https://twitter.com/mkulimambunifu>



+255 785 496 036



Picha: MKM

Mbuzi aliyeathiriwa na ndui

kuacha kabisa kufanya uzalishaji wa mbuzi na kubadili upepo.

Katika toleo hili, tutaangalia kidogo kuhusu ugonjwa wa ndui ya mbuzi ambao umegundulika kuwepo mkoani Tarime kwa hivi karibuni, hivyo wafugaji hawana budi kuufahamu na kujua ni kwa namna gani wanaweza kuudhibiti.

Yaliyomo

Mnyororo wa thamani	2
Ufugaji wa nguruwe	3
Zao la soya	7



Zao la soya

Mpendwa mkulima

Heri ya mwaka mpya msomaji wa Jarida la Mkulima Mbunifu. Kipenga kimeshapulizwa na ni matumaini yetu kuwa mwaka umeuanza salama kabisa, na hatuna budi kukupa hongera pia kwa kuanza mwaka huu ukiwa mzima. Vinginevyo basi yote ni kushukuru tu.

Pamoja na hayo yote, tuna imani kuwa mikakati uliyoiweka kwa ajili ya kufunga na kufungua mwaka hakika imeanza kutekelezwa barabara.

Endapo haukuweza kutwaka mipango thabiti kuwa ni kipi utanza kutekeleza kwa mwaka huu, basi ni vyema sasa ukaweka mipango hiyo na kuitekeleza kwa kuwa muda hautakungoja usipojipanga vizuri.

Kuna msemu usemao, mipango thabiti, husababisha mafanikio na utendaji thabiti. Hivyo hakikisha unakuwa na mipango thabiti itakayokuwezesha kufikia malengo yako.

Pamoja na kujipanga, ni muhimu sana kutafuta na kupata taarifa sahihi itakayokusaidia katika shughuli zote ambazo umepanga kutekeleza kwa mwaka mzima.

Endapo unahitaji kuzalisha mazao kwa ajili ya chakula cha familia na biashara, basi tafuta kupata taarifa na elimu sahihi juu ya zao husika. Hii ni pamoja ufahamu wa mbegu bora, namna ya kupanda, matunzo na namna ya kukabiliana na wadudu na magonjwa endapo yatajitokeza.

Sambamba na mazao, fanya hivyo vivyo kwa uzalishaji wa mifugo ya aina mbalimbali. Na inapofikia msimu wa kuvuna na kuuza, usikurupuke.

Hakikisha unapata taarifa sahihi za soko pamoja na bei halisi ya bidhaa au mazao uliyozalisha shamnani mwako, na usiuzue kwa kulazimishwa na wachuuzi.

Ni wazi kuwa endapo utapa taarifa sahihi juu ya yote unayokusudia kufanya, mafanikio nayo ni dhahiri. Tumia vyanzo vya kuaminika, pamoja na wataalamu wenye uzoefu kwa ajili ya kukusaidia kufikia malengo.

Fahamu kuhusu mnyororo wa thamani katika mazao ya kilimo hai

Mimi ni msomaji wa MkM, kwa muda mrefu na nimepata ushawishi Zaidi kufanya kilimo hai. Napenda kufahamu kwa undani kuhusu dhana nzima ya mnyororo wa thamani-Msomaji MkM Bumbuli Tanga.

Ayubu Nnko

Mnyororo wa thamani ni mtiririko wa shughuli zote zinazofanywa katika uzalishaji hadi kumfikia mlaji. Mtiririko huu hujumuisha shughuli mbalimbali hadi kufika kwa mlaji, ambae ni mtumiaji wa mwisho wa bidhaa au zao lililozalishwa. Kila kazi inayofanywa kutimiza mzunguko mzima huongeza thamani ya zao au bidhaa husika.

Mnyororo wa thamani hujumuisha kazi mbalimbali kama vile uzalishaji, usafirishaji, usindikaji, uhifadhi, upangaji wa madaraja, kufungasha na masoko.

Uzalishaji

Kazi hii hufanyika kwa kufuata taratibu zote za uzalishaji wa mazao kwa kufuata kanuni na taratibu zote za uzalishaji wa zao husika. Hii ni pamoja na kutumia mbegu sahihi, kupanda kwa wakati, matunzo sahihi, kwa kufuata kanuni zote muhimu katika kilimo hai, ikiwa ni pamoja na kutotumia kemikali na kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Usafirishaji

Hii ni moja ya kazi muhimu sana katika mnyororo wa thamani, kwa kuwa lengo lake ni kusogeza bidhaa kwa mlaji na kurahisisha huduma. Hali hii pia huongeza thamani, na ndiyo sababu bei ya shambani hutofautiana na bei ya sokoni.

Ni muhimu kwa wasafirishaji kuzingatia kanuni husika ili bidhaa ifike sokoni ikiwa bado na ubora unaostahili.



Mazao ya bustani yakilimwa vizuri mkulima hupata mavuno bora

Uhifadhi

Ni muhimu wakulima kuhakikisha kuwa wana utaratibu mzuri wa kuhifadhi mazao yao kunapokuwa na mazao mengi. Mkulima ajifunze njia mbalimbali za uhifadhi kwa matumizi ya baadae. Mfano ukaushaji wa matunda.

Uhifadhi husaidia upatikanaji wa zao au bidhaa husika katika kipindi ambacho yasingepatikana. Ni muhimu kuzingatia kanuni sahihi za uhifadhi bila kutumia kemikali.

Zingatia usafi wa mazingira na viwango vinavyokubalika. Usipohifadhi kwa usahihi ni rahisi kushusha thamani ya mazao husika.

Upangaji katika madaraja

Hii ni moja ya hatua muhimu sana, ambayo humsaidia mkulima au mzalishaji kupata bei tofauti kwa mazao au bidhaa aliyozalisha. Hii ni kwa sababu mazao yenye ubora Zaidi ni rahisi kuuzika kwa bei ya juu, kuliko yale ambayo yana ubora hafifu. Mkulima anaweza kupanga bei awezavyo kulingana na madaraja na ubora wa bidhaa zake.

Usindikaji

Hii ni hali ya kubadili bidhaa yako

kutoka katika hali moja na kuwa na thamani Zaidi. Ni mwanzo wa kufanya bidhaa kuwa na maisha marefu Zaidi.

Mfano ni ukaushaji wa mbogamboga na matunda kwa matumizi ya baadae. Hali hii hutoa fursa ya bei Zaidi kwa bidhaa husika na ajira kwa watakoajumuishwa katika kazi hiyo.

Ufungashaji

Hii ni hatua inayofuata baada ya usindikaji. Shughuli hii hujumuisha ufungashaji katika viwango tofauti. Hii inasaidia walaji wenye uwezo na uhitaji tofauti kuweza kupata huduma hiyo. Pia hali hii husaidia kuweka bidhaa katika hali ya kuwa na umbo sahihi na kuvutia.

Hatua hii ni hujumuisha vipimo na viwango vinavyokubalika kimataifa. Hii ni pamoja na uwekaji wa nembo yenye taarifa sahihi.

Soko

Hii ni hatua ya mwisho kabisa katika mnyororo wa thamani. Hapa muuzaji na mnunuzi hukutana na kufanya biashara. Soko la bidhaa unazozalisha itategemea ni jinsi gani ulivyozingatia hatua zote muhimu kama ilivyoielezwa katika maelezo na hatua za awali.

Inaendelea Uk 7 ➔

Mkulima Mbunifu ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa kila mwezi na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni moja wapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekele-



zwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linasambazwa kwa wakulima bila malipo. *Mkulima Mbunifu* linafadhiliwa na Biovision - www.biovision.org. **Wachapishaji** African Insect Science for Food and Health (icipe), S.L.P 30772 - 00100 Nairobi, KENYA, Simu +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org



Mpangilio Ibrahim Isack, +255 676 293 261
Zenith Media Ltd
Mhariri Msaidizi Flora Laanyuni
Mhariri Ayubu S. Nnko
Mhariri Mkuu Venter Mwongera
Anuani *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction block) S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
Ujumbe Mfupi Pekee: 0785 496 036, 0766 841 366
Piga Simu 0717 266 007, 0785 133 005
Barua pepe info@mkulimambunifu.org, www.mkulimambunifu.org

Hakikisha nguruwe wanapata lishe bora na kwa wakati

Chakula bora kwa Nguruwe ni moja ya suala muhimu sana kwenye dhana nzima ya ufugaji wa Nguruwe wenye tija na faida kwa mfugaji.

Agustino Chengula

Chakula cha nguruwe kinagharimu kama asilimia sabini ya garama zote za ufugaji.

Kati ya matatizo mengi yanayosababisha tija na ufanisi duni wa uzalishaji wa nguruwe yanatokana na lishe duni. Endapo wakipatiwa lishe bora, tija na ufanisi wa uzalishaji utakuwa mkubwa hivyo kuongeza faida kwa mfugaji.


Baadhi ya faida za kulisha lishe bora kwa nguruwe

- Lishe bora huharakisha ukuaji wa haraka wa nguruwe, hivyo kupata uzito unaohitajika kwa kipindi kifupi.
- Lishe bora hupunguza gharama za ufugaji na hivyo kuongeza faida kwa mfugaji kwa sababu nguruwe atahitaji kiasi kidogo tu cha chakula na atachukua muda mfupi kupata uzito mkubwa.
- Lishe bora itapunguza maambukizi ya magonjwa.
- Lishe bora huongeza kiasi cha mayai yatakayoivishwa na nguruwe jike na hivyo kuongeza idadi ya watoto watakozaliwa.
- Lishe bora huongeza kiasi cha maziwa yatakayotengenezwa na mama nguruwe kwa ajili ya watoto hivyo kuwafanya wawe na afya bora itakayo wawezesha wakue haraka na kupunguza idadi ya vifo kwa watoto.
- Lishe bora inaongeza ufanisi wa madume ya nguruwe na hivyo kuongeza uwezo wa kupanda.

Viini lishe muhimu kwenye lishe ya nguruwe

Nguruwe wanauwezo wa kula aina nyingi za vyakula lakini vyenye uwezo wa kumeng'enywa kwa urahisi. Chakula cha Nguruwe kilichokamilika kinahitaji kuwa na mchanganyiko wa viini lishe vitano, navyo ni

Vyakula vyenye kutia nguvu mwilini (vyakula vyenye asili ya wanga) kama vile pumba za mchele, pumba za



Nguruwe wanahitaji kupewa lishe bora ili waweze kupata afya nzuri

mahindi, pumba za ngano, machicha ya pombe yaliyokaushwa, mihogo, viazi vitamu, viazi mvingo, miwa, ndizi mbichi, zilizoiva au zilizopikwa na makombo ya vyakula vya asili vya wanga.

Vyakula vya kujenga mwili (Vyakula vyenye asili ya protini) ni pamoja na mashudu ya alizeti, mashudu ya pamba na mawese, unga wa dagaa/samaki, damu iliyokaushwa, soya.

Vyakula vya asili ya madini

Chumvi ya mezani, chokaa ya mifugo (Limestone), mifupa iliyosagwa (bone meal), madini maalum ya nguruwe (Pig mix), madini mchanganyiko (mfano maklic), madini ya chuma (hasa kwa watoto wa nguruwe).

Vyakula vya asili ya vitamini

Hivvi ni pamoja na majani mabichi laini, mbogamboga, matunda k.m parachichi, maembe, mapapai n.k, viungo mboga kama nyanya, bilinganya, au mchanganyiko maalumu yenye viasilia vya vitamini kama vile premix.

Maji

Hii ni lishe muhimu kwenye chakula cha nguruwe, ila tofauti na viini lishe vingine vilivyotajwa hapo juu ambapo nguruwe anapewa kwa vipindi/muda na kiwango maalum, maji yanahitajika kwa nguruwe muda wote. Mahitaji ya maji ya kunywa kwa nguruwe ni kama ifuatavyo:-

- Nguruwe anayenyonyesha lita 20 kwa siku
- Nguruwe aliyeachishwa kunyonyesha lita 5 kwa siku
- Nguruwe wanaokuzwa na

kunepeshwa wenye kilo 20 hadi 90 lita 5 kwa siku

- Watoto wa nguruwe lita 1 kila mmoja

Tengeneza chakula cha nguruwe

Ni muhimu kutengeneza chakula kwa ajili ya kulisha nguru na wakati wa kutengeneza chakula cha nguruwe hakikisha unazingatia yafuatayo:

- Mchanganyiko wako uwe na viinilishe vinne vilivyotajwa hapo mwanzo
- Chagua aina ya viinilishe vinavyoweza kupatikana kwa urahisi na bei nafuu kwenye mazingira yako
- Aina ya mchanganyiko wa chakula ni muhimu uzingatie mahitaji ya nguruwe kama umri (kama vile nguruwe wanaonyonya, waliochishwa kunyonya, wanaokua, na wanaonyonyesha)

Kiasi na namna ya kulisha

Nguruwe wanahitajika kulishwa aina sahihi ya chakula mara mbili (asubuhi na mchana) au zaidi kwa siku.

Kiwango/kiasi cha kulisha kwa nguruwe wa aina na rika tofauti hutofautiana hivyo ni muhimu kujua kiasi sahihi cha kulisha nguruwe husika kwa siku.

Wafugaji wanashauriwa kuwapatia nguruwe vyakula vyao vya asili kama vyakula vya ziada mfano, majani mabichi laini, majani ya mboga, mbogamboga, matunda kama maparachichi, majani ya viazi.

Zalisha na sindika alizeti kwa kuongeze

Zao la alizeti hulimwa kwa wingi kwa ajili ya chakula na biashara hasa katika mikoa ya Shinyanga, Dodoma, Iringa, Tabora, Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Arusha, Manyara na Rukwa.

Flora Laanyuni

Wakulima walio wengi wamekuwa wakizalisha alizeti bila kuweka na kufuata hatua sahihi zinazohitajika kwa ajili ya kilimo cha zao hilo, huku wakipata mavuno hafifu na yasiyokuwa na ubora.

Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa uzalishaji

Mbegu

Mkulima ni lazima achague mbegu inayovumilia magonjwa, wadudu, inayotoa mavuno mengi na yenye kiwango kikubwa cha mafuta.

Vilevile ni lazima kuchagua aina ya mbegu ambayo hukomaa kwa wakati mmoja ili kurahisisha uvunaji.

Mbolea

Ni lazima udongo urutubishwe kwa kutumia mbolea za mboji au samadi iliyoiva vizuri ili kupata mazao mengi na yenye ubora.

Wadudu na magonjwa

Alizeti hushambuliwa sana na magonjwa ya majani, mizizi na masuke, ambayo husababisha upungufu wa mavuno, hivyo ni muhimu kuyadhibiti ili kupata mavuno mengi na bora.

Pia ndege hupunguza mavuno kwa kiasi cha asilimia 50 au zaidi. Njia ya udhibiti wa ndege ni kwa kuweka mitego ya kuwafukuza na kupata

mbegu zinazokomaa mapema.

Upandaji

Alizeti ipandwe katika shamba lililoandaliwa kwa kulimwa vizuri ili kuweza kuruhusu mbegu kukua bila shida. Nafasi kati ya shimo na shimo iwe sentimita 30 na nafasi kati mstari na mstari iwe ni sentimita 75.

Maandalizi kabla ya kuvuna

Kugua shamba

Kagua shamba ili kuona kama alizeti imekomaa vizuri. Alizeti hukomaa kati ya miezi minne hadi sita tangu kupanda na wakati huo punje huwa na unyevu wa asilimia 25.

Ni muhimu kuvuna alizeti mapema mara tu inapokomaa ili kuepuka mashambulizi ya panya, mchwa na ndege waharibifu.

Dalili za alizeti iliyokomaa

Suke hubadilika rangi kutoka manjano na kuelekea kuwa nyeusi. Vilevile viua vya pembeni mwa suke hunyauka na hubadilika kutoka rangi ya manjano na kuwa ya kahawia.

Vifaa vya kuvunia na kubebea

Vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kuvuna alizeti na kubebea kutoka shambani ni kisu, vikapu, magunia na matenga.

Vifaa vya kukaushia

Mara baada ya kuvuna alizeti inahitaji kukaushwa hivyo vifaa kama vile maturubai, mikeka na kichanja bora cha kukaushia huhitajika.

Vyombo vya usafiri kutoka shambani

Matoroli, tela ya trekta, mikokoteni



zao la alizeti lililozalishwa kwa

ya kukokotwa na wanyama pamoja na magari, huweza kutumika kama vyombo vya kusafirishia alizeti.

Kuvuna

Alizeti huvunwa kwa kutumia mikono, ambapo suke hukatwa kwa kutumia kisu au mashine (combine harvester) hutumika kuvunia alizeti katika nchi zinazolima alizeti kwa wingi.

Masuke ya alizeti huwekwa kwenye vikapu ambavyo hutumika kusomba alizeti ndani ya shamba kisha alizeti kufungashwa kwenye magunia na kusafirishwa tayari kwa ajili ya kukaushwa.

Kukausha

Kuna hatua mbili za kukausha alizeti ambazo ni kukausha masuke na kukausha mbegu za alizeti.

Kukausha masuke

Masuke hutandazwa kwenye kichanja bora katika kina kisichozidi sentimita 30 ili yaweze kukauka vizuri.

Vilevile masuke huweza kukaushwa kwa kutandazwa kwenye maturubai, mikeka au sakafu iliyo safi.

Lengo la hatua ya kukausha



Mavuno ya alizeti

kuweza thamani na ubora



Picha: IN

kwa ubora hutoa mavuno mengi

masuke ni ili kuweza kurahisisha upuraji.

Kupura

Upuraji hufanyika baada ya kuhakikisha kuwa masuke ya alizeti yamekauka vizuri na masuke hayo hupurwa kwa kutumia mikono, ambapo mbegu hutenganishwa kwa kupiga masuke taratibu kwa kutumia mti.

Ni muhimu kupiga masuke taratibu ili kuepuka kupasua mbegu, lakini pia yapurwe kwenye kichanja bora, maturubai au mikeka.

Kukausha mbegu

Mbegu za alizeti hukaushwa juani kwa kutandazwa kwenye vichanja bora, maturubai, mikeka au sakafu safi.

Mbegu itandazwe katika kina kischozidi sentimita 4 ili ziweze kukauka vizuri.

Lengo la hatua hii ni kukausha mbegu baada ya kupura ili kufikia kiwango cha unyevu kinachotakiwa kwa hifadhi salama ambacho ni asilimia 8.

Jinsi ya kutambua mbegu zilizokauka vizuri

Mbegu zilizokauka maganda yake hutoka kwa urahisi pindi zinapofikichwa.

Mbegu zilizokauka hutoa mlio mkali zinapomiminwa kwenye chombo kama vile debe na mbegu hizo hung'ara.

Mbegu zilizokauka vizuri zinapowekwa kwenye kipima unyevu, basi kipimo hicho huonesha asilimia 8.

Kupepeta na kupembua

Kazi hii hufanyika ili kuondoa takataka kama vile mawe, wadudu, mapepe, mbegu zilizooza na kupasuka.

Mbegu za alizeti hupepetwa kwa kutumia ungo au mashine zinazoendeshwa kwa mkono, injini au umeme.

Mashine hizi zina uwezo wa kupepeta na kupembua kilo 60 hadi 350 kwa saa kutegemea aina ya mashine inayotumika.

Kuhifadhi

Alizeti iliyopurwa huhifadhiwa katika hali ya kichele kwenye maghala bora, yaani vihenge, sailo au bini. Alizeti ya kuhifadhi kwenye maghala ya nyumba ifungashwe kwenye magunia na ipangwe kwenye gala kwa kupishanisha.

Ili kurahisisha kazi ya kukagua ghala, acha nafasi ya mita moja kutoka kwenye ukuta na ziba sehemu zote za ghala ili kuzuia panya kuingia.

Panya hupenda sana kula mbegu za alizeti na husababisha upungufu mkubwa wa punje ambao husababisha upotevu wa asilimia 30 kwa kipindi cha iezi mitatu tu ya hifadhi.

Asilimia ya upotevu inaweza kuwa kubwa Zaidi kutegemea idadi

ya panya na upatikanaji wa vyakula vingine kwa wakati huo.

Matumizi ya mbegu za alizeti

Mbegu za alizeti hasa zenye mistari zinaweza kuliwa baada ya kukaangwa au kukaushwa na pia zinatumiwa katika utengenezaji wa mikate. Mbegu hizo husindikwa pia ili kupata mafuta.

Kusindika mbegu za alizeti kupata mafuta

Vifaa

Vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya usindikaji ni pamoja na mashine ya kukamua mafuta, chujio safi, ndoo, vifungashio, sufuria na mizani.

Malighafi

Malighafi ni pamoja na mbegu zenyewe za alizeti, maji safi na salama na chumvi.

Njia ya kukamua alizeti

Chagua mbegu bora za alizeti kisha zianike kwenye jua kwa muda wa saa 1 hadi 2.

Weka kwenye mashine ya kukamulia au ram na kamua mafuta kisha chuja kwa kutumia kitambaa safi au chujio safi.

Pima mafuta yaliyokamuliwa na ongeza maji na chumvi, yaani katika lita 10 za mafuta weka lita moja ya maji na gramu 200 za chumvi.

Weka mafuta kwenye chombo cha kuchemshia (sufuria) na chemsha hadi maji yote yaishe.

Sauti ya kuchemsha ikiisha ni dalili kuwa maji yamekwisha hivyo ipua na acha yapoe kisha chuja kwa kitambaa safi au chujio.

Fungasha kwenye vyombo safi na vikavu na vyenye mifuniko kisha weka lakiri na lebo.



Picha: IN

Mafuta ya alizeti

Ndui ya mbuzi: Ugonjwa hatari usio na tiba

Ugonjwa wa ndui ya mbuzi husababishwa na virusi na ugonjwa huu unaweza kuandamana au kuja sambamba na nimonia.

Flora Laanyuni

Ugonjwa huu ni hatari sana kwani kati ya kila mbuzi 100 wanaogua ugonjwa huu, kiasi cha mbuzi wapatao 80 wanaweza kufa.

Dalili zake

- Mbuzi hupatwa na homa kali na hata kutoa makamasi.
- Wakati mbuzi akiwa amesimama huonesha kupinda mgongo.
- Manyoya ya mbuzi pia husimama tofauti na hali ya kawaida.
- Mbuzi hutokwa na vipete vidogovidogo mwilini ambavyo baadaye hukauka na kufanya utando unaodumu kwa wiki 3 hadi 4.

Jinsi ya kuzuia

Mbuzi wachanjwe dhidi ya ugonjwa huu mara moja kwa mwaka kwa kuwatumia wataalamu wa mifugo na si vinginevyo.



Mbuzi mwenye ugonjwa wa ndui hutokwa na vipete hata mdomoni

► Inatoka Uk. 3.... Hakikisha nguruwe wanapata lishe bora na kwa wakati

Ulishaji wa Maziwa ya Kwanza

Mara tu baada ya kuzaliwa hakikisha kuwa vitoto vinanyonya maziwa ya kwanza. Maziwa haya ni muhimu kwani yana viinilishe vya kujenga mwili, kuleta nguvu na kuongeza kinga dhidi ya maradhi.

Kama mama amekufa mara tu baada ya kuzaa na hakuna nguruwe mwingine anayeweza kuwanyonyesha, wapewe maziwa ya kwanza ya ng'ombe. Endapo yatakosekana wapewe mchanganyiko maalum wa maziwa ya ng'ombe.

Joto

Watoto wa nguruwe huzaliwa bila manyoya na huwa hawana mafuta mengi ya kutosha kuwapatia joto mwilini. Kwenye sehemu za baridi ni jambo la muhimu kuwapatia joto kwa kutumia umeme au chemli.

Kuzuia Upungufu wa Damu

Nguruwe huzaliwa wakiwa na upungufu wa madini ya chuma halikadhalika maziwa ya mama yao huwa na upungufu wa madini hayo, hivyo wasipopatiwa madini hayo hupata upungufu wa damu, hudhoofika na hatimaye hufa.

Kulisha Chakula cha Kwanza

Watoto wapewe chakula maalum kidogo kidogo kuanzia siku ya kumi baada ya kuzaliwa. Chakula hiki kinatakiwa kiwe na viinilishe vya kujenga mwili, kuleta nguvu na kuzuia maradhi. Wakiwa na umri wa wiki tatu wapewe gramu 450; wiki ya nne na ya tano wapewe gramu 680 kwa nguruwe kwa siku. Endelea kuwapa chakula hiki mpaka siku ya kuachishwa kunyonya, na vile vile wapewe maji kwa wingi.

Kuhasi

Watoto madume ambao hawahitajiki kwa ajili ya kuzalisha wahasiwe wakiwa na umri kati ya wiki tatu hadi sita.

Nguruwe waliohasiwa huwa wapole, hunenepa haraka, huwa na nguvu na wazito kwa hiyo wanafaa kwa nyama na mafuta. Muone mtaalam wa mifugo kwa ajili ya kuhasi nguruwe wako.

Vitambulisho

Ngumwe hupewa vitambulisho kabla ya kuwatenganisha na mama yao kwa kuwaweka nambari kwenye masikio. Unashauriwa kumuona mtaalam wa

mifugo akupe ushauri wa jinsi ya kuweka vitambulisho hivyo.

Kutenganisha watoto na mama yao. Watoto wakifikia wiki nane watenganishe na mama yao. Mama ahamishwe kwenye chumba na kuwaacha watoto ili kupunguza mgutusho wa kuhamia mahali pengine. Unapowatenganisha hakikisha unawapa dawa ya minyoo, unawakinga dhidi ya magonjwa na kuwatibu mara wanapougua.



Mahindi ni moja ya malighafi zinazotumika kutngeneza lishe ya nguruwe

Tambua wadudu, magonjwa na wanyama waharibifu wa soya

Kama ilivyo kwa mazao mengine, zao la soya pia lina aina za wadudu na magonjwa ambayo huathiri zao hilo shamba lisipotunzwa vizuri, na wakati mwingine hutokana na msimu na hali ya hewa.

Patrick Jonathan

Kuna baadhi ya wadudu na magonjwa yanayoshambulia zao la soya.

Wadudu

Kwa sasa nchini Tanzania, soya haishambuliwi sana na wadudu kama ilivyo sehemu nyingine ambako zao hilo hulimwa kwa wingi.

Hata hivyo endapo wadudu watatokea mkulima anashauriwa kuwasiliana kwa haraka na mtaalamu wa kilimo alie karibu, na kutumia dawa zisizo na madhara.

Tofauti na mazao kama mahindi na maharagwe, hakuna wadudu waharibifu wa soya ghalani.

Zao hilo linaweza kutunzwa kwa muda mrefu ghalani bila kuwa na athari za wadudu. Kwa mkulima na wafanyabiashara, kutokuwepo wadudu waharibifu ghalani kunapunguza gharama za utunzaji hadi bei nzuri itakapofikiwa.

Magonjwa

Kama ilivyo kwa wadudu, magonjwa ya soya ni machache. Hata hivyo magonjwa ambayo hutokea kwa nadra ni yale yanayotokana na vimelea vya ukungu na bakteria.



Soya iliyozalishwa kwa udhibiti mzuri wa magonjwa na wadudu

Magonjwa hayo huenezwa kwa mbegu, masalia ya mimea shambani na wadudu mafuta.

Hivyo ni bora kwa mkulima kuzingatia kanuni za kilimo bora au kupata ushauri wa kitaalamu ili kuepukana na magonjwa hayo.

Njia mojawapo ya kuzuia kuenea kwa magonjwa katika zao la soya ni kupanda mbegu safi na zilizopendekezwa kwa eneo husika. Aidha, panda kwa mzunguko

(crop rotation) kwa kutumia mazao yasiyoshambuliwa na magonjwa ya soya kama alizeti na mahindi.

Wanyama waharibifu

Kwa kawaida soya hupendwa sana na panya wa shambani na ghalani. Wanyama wengine ni pamoja na sungura, paa, swala, n.k.

Mkulima anashauriwa kutumia mbinu na njia mbalimbali zikiwemo za asili, kukabiliana na wanyama hao bila kuharibu mazingira.

► Inatoka Uk. 2..... Mnyororo wa ongezeko la thamani

Uuzaji katika soko pia hutegemea Sanaa ya muuzaji ikiwa ni pamoja na kuifahamu vizuri bidhaa yake. Kwa mfano; Muuzaji wa bidhaa za kilimo hai ni lazima aelewe na kueleza kwa ufasaha kabisa upekee uliopo katika bidhaa zinazotokana na kilimo hai.

Unaweza kuongeza thamani ya bidhaa zako kwa kuweka walaji katika madaraja, kutangaza bidhaa zako, pamoja na ulinganifu wa uwezo wa kununua.

Muhimu: Usafi ni nguzo muhimu katika mnyororo wa thamani. Zingatia usafi wa bidhaa na mazingira wakati wote. Badili muonekano wa eneo na bidhaa kila wakati.

Nivyema kukumbuka na kuzingatia kuwa kila anaeshiriki katika hatua moja wapo, huongeza

thamani na hivyo kuvutia ongezeko la gharama, hivyo ni muhimu kufikiri namna nzuri na bora inayoweza kufupisha mnyororo, ili usiwe mrefu sana na kusababisha bei ya bidhaa kuwa kubwa sana.

Changamoto

Kunahitajika umakini wa hali ya juu sana katika kulinda ubora wa mazao ya kilimo hai, ili kutokuchanganya bidhaa zako na zile zilizozalishwa kwa kutumia kemikali.

Kuna changamoto kubwa kwa usafirishaji, kwa wanaosafirisha kutoka vijijini, kwani mara nyingi huishia kuchanganya mazo yao na yale yaliyozalishwa kwa kutumia kemikali.

Kwa maelezo Zaidi juu ya mnyororo

wa ongezeko la thamani, unaweza kuwasiliana na wawezeshaji wa idara ya masoko kutoka SAT, Akle Mbaye +255763987536, na Frank Kimaro +255742 411 655



Duka la mazao ya kilimo hai (SAT)

Jarida la MkM Limetuamsha kuanzisha miradi mbalimbali

Ilikuwa kama ajabu kwetu, maana kila tulipofungua ukurasa, tulizidi kuwa na shahuku ya kuanzisha na kujihusisha katika mradi mpya. Yale yaliyoandikwa katika toleo la 59, ndiyo yametufanya leo tutambulike na kufanya haya.

Ayubu Nnko

Ndivyo alivyoanza kueleza mwenyekiti wa kikundi cha Changamoto, Bw. Swaladen Omar Heri, kutoka katika kijiji cha Mfumbwe, kata ya Mkuyuni Wilaya ya Morogoro Vijijini.

Wakiwana furaha huku wakionesha hatua ya mafanikio waliyonayo baada ya kusoma jarida la MkM, wanachama wa kikundi hicho chenye wanachama 26 wanasema mengi ambayo wameyafanya yamekuwa yakitiwa msukumo na jarida la MkM, huku wakipata usaidizi wa mafunzo ya vitendo kutoka SAT.

Pamoja na kuimarika katika utunzaji na uzalishaji wa mazao ya viungo baada ya kusoma jarida la MkM toleo la 59, wakulima hawa wameweza kuchimba bwawa la samaki na kuanza mradi huo baada ya kusoma kwa kina maelezo juu ya ufugaji wa samaki kupitia jarida la MkM.

Swaladen anasema kuwa wakiwa katika majadiliano ya pamoja katika kikundi chao kama ilivyo ada, kila mmoja aliguswa na kuvutiwa Zaidi na mada ya ufugaji wa samaki, na ndipo walipoamua kwa pamoja kuanzisha mradi huo kwa kufuata maelekezo yaliyomo katika jarida la MkM.

Bwawa hilo lenye ukubwa wa mita 10 kwa 10 limechimbwa na kujengwa kwa nguvu kazi za wanakikundi wenyewe.

Ubunifu

Pamoja na kuchimba bwawa hilo, kikundi hicho kimefanikiwa kutengeneza miundo mbinu ya maji kutoka umbali wa mita 250 kwa kutumia mianzi.

Wanaeleza kuwa kauli mbiu ya Mkulima Mbunifu kuwa wakulima na wafugaji watumie malighafi zinazopatikana katika maeneo yao, kutatua changamoto zinazowakabili, iliwasukuma kubuni bomba la maji kwa kutumia mianzi ambayo walikata na kupasua, kisha kuunganisha kama bomba hadi kufika katika bwawa.



Picha: MkM

Kikundi cha changamoto wameanzisha mradi wa ufugaji wa samaki baada ya kusoma MkM

Malengo

Mwenyekiti wa kikundi cha changamoto anaeleza kuwa pamoja na mambo mengine, lakini malengo makuu ya kikundi hicho kwa sasa ni pamoja na;

- Kuongeza kipato kupitia ufugaji wa samaki.
- Kupata lishe bora kwa ajili ya familia zao.
- Kupata elimu Zaidi ya ufugaji na ufungashaji.
- Kupanua mradi wa ufugaji samaki kwa kujenga mabwawa Zaidi.

Changamoto

- Mtaji mdogo wa kukuza shughuli zao kwa haraka
- Kufahamu ni aina gani ya samaki katika eneo lao inaweza kuwapatia faida kwa haraka.

Uzalishaji viungo

Mradi wa Viungo ni moja ya shughuli kuu za kikundi cha Changamoto

Pamoja na mambo mengine kikundi cha changamoto kinajishughulisha na uzalishaji wa mazao ya viungo kama vile karafuu, mdalasini, pilipili manga, na Tangawizi.

Katibu wa kikundi hicho Bw. Idd Rashidi Manyasi anaeleza kuwa walihamasika kufanya aina hiyo ya kilimo baada ya kugundua kuwa wazalishaji wa mazao hayo ni wachache, ulimaji wake ni wa muda mrefu na kina faida endelevu.

Halikadhalika pato linalotokana na

uzalishaji wa mazao hayo ni kubwa, Taifa pia linapata pato kwani soko la mazao ya viungo ni kubwa ndani na nje ya nchi ya Tanzania.

Idd anaeleza kuwa walihamasika Zaidi baada ya kuona kikundi katika kijiji jirani wakifaidika na uzalishaji wa mazao hayo, na baada ya hapo walipata magunzo kutoka SAT, huku wakipata msukumo Zaidi kwa kusoma MkM.

Malengo

- Hadi kufikia 2020 wawe wamepunguza hali ya umaskini kwa mwanachama mmoja mmoja.
- Wawe wameboresha utunzaji wa mazingira.
- Wawe wameongeza uzalishaji.

Uzalishaji viungo Uluguru

Huu ni mradi wa miaka mitatu unaofanya kazi kwa kushirikiana na vikundi vya wakulima na kusimamiwa na SAT. Mradi huu unafanya kazi kwa kufuata misingi na teknolojia ya kilimo hai.

Mradi wa viungo unajumuisha takribani vikundi 20 vyenye wastani wa wakulima 500 wanaokusudiwa kufaidika na mradi huo.

Changamoto

Mtawanyiko wa vikundi huku baadhi ya maeneo yakiwa hayafikiki kwa urahisi.

Kwa maelezo Zaidi juu ya mradi wa uzalishaji viungo uluguru unaweza kuwasiliana na SAT kwa namba +255 754 925 560